
Ghorofa ya 7, Jengo la LAPF Pension Fund, Mkabala na Kijiji cha Makumbusho, Kijitonyama
S.L.P. 72175, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255-22 2923513-18; Nukushi: +255-22 2923519
Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI

TAARIFA KWA UMMA

11/06/2017

(Imetolewa chini ya kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania na kifungu cha 8 cha Sheria ya Umeme, Sura ya 131 ya Sheria za Tanzania)

TAARIFA inatolewa kwa umma kwamba kufuatia maombi ya kampuni ya uzalishaji umeme ya INDEPENDENT POWER TANZANIA LIMITED (IPTL) (“Mwombaji”) kuomba kuongezewa muda wa leseni yake ya kuzalisha umeme kwa kipindi cha miezi 55 kutokea tarehe 15 Julai 2017, EWURA, zaidi ya hatua nyingine za kiudhibiti, iliwasiliana na Wizara ya Nishati na Madini ili kupata maoni yake kwa mujibu wa kifungu cha 7 (3) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Wizara ya Nishati na Madini imetoa mapendekezo ya kuwapo na mashauriano zaidi kati ya Wizara, EWURA na wadau mbalimbali wa sekta ndogo ya umeme kabla ya kuendelea na mchakato wa maombi ya Mwombaji.

Kutokana na maoni hayo, EWURA inasitisha mchakato wa kushughulikia maombi ya leseni ya Mwombaji ikiwa ni pamoja na upokeaji wa maoni/mapingamizi dhidi ya maombi hayo mpaka hapo yatakapotolewa maelekezo mengine.

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)
Ghorofa ya 7, Jengo la LAPF Pension Fund Towers,
Mkabala na Kijiji cha Makumbusho, Kijitonyama ,
S. L. P 72175, Dar es Salaam
Nukushi: +255 (022) 2923519
Simu: +255 (22) 2923513-18
Barua Pepe: info@ewura.go.tz, Tovuti: www.ewura.go.tz